

Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa viwandani. **Picha ya Maktaba.**

**HABARI ZAIDI**

-Chama cha Nishati ya Jua Tanzania (TASEA) hivi karibuni kilalamika kwamba kuna vifaa bandia visivyokuwa na viwango vya kunasia nishati ya jua katika maduka mbalimbali nchini.

-Mapema mwaka huu, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) walipiga marufuku dawa bandia ya malaria ya Metakelfin na kutaka wauzaji kurejesha dawa hizo kwa wauzaji wao.

-Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Tume ya Ushindani nchini (FCC), Frank Mdimi anasema: "Kununua bidhaa bandia kunasababisha bidhaa hizo kuendelea kuwapo sokoni, bidhaa hizi ni rahisi, lakini ni za viwango vya chini kiteknolojia.

# Sheria mpya kunusuru walaji dhidi ya bidhaa bandia

**Bidhaa bandia ni zile zenye viwango hafifu ambazo zinaua viwanda vya wazalendo.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Juni 15,2012 Rais Jakaya Kikwete alitia saini muswada wa marekebisho ya sheria za biashara. Miongoni mwa sheria ambazo zimefanyiwa marekebisho ni sheria ya bidhaa (CAP 85).

Sheria hiyo mpya inaelezea bidhaa bandia ambazo zimegushiwa na kuuzwa kiharamia katika njia ambazo siyo halali kisheria, na kazi za kughushi ambazo huzalisha bidhaa bandia. Sheria hiyo inamwona mtu anayemiliki mali za kughushi ana hatia.

Kwa miaka mingi Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) limekuwa likilalamika jinsi bidhaa bandia zinavyoathiri viwanda vya ndani.

Kutokana na kuwapo kwa sheria hiyo mpya inaaminika kwamba itasaidia kupunguza sana tatizo la bidhaa bandia hasa itakapoanza kutumika. Hivi sasa bidhaa bandia zinaathiri kwa kiwango kikubwa ufanisi wa viwanda vya ndani.

**Bidhaa bandia ni kikwazo**

Tume ya ushindani nchini (FCC) imekabidhiwa dhamana ya kukabiliana na bidhaa bandia nchini Tanzania kwa kuhakikisha kwamba sheria ya bidhaa inatekelezwa. Hata hivyo FCC pamoja na kupewa dhamana hiyo inaonekana kutokuwa makini hasa kutokana na ukweli kwamba hadi Julai 30, mwaka huu haijaweka taarifa mpya kuhusu marekebisho ya sheria hiyo.

Tovuti hiyo competition.or.tz bado ina taarifa za sheria ya zamani na kwa msingi huo imeshindwa kutoa msukumo wa uelewa kwa watu kuhusu haja ya kukabiliana na bidhaa bandia kwa nguvu zote.

Hivi karibuni FCC ilikamata mabomba bandia 728 yenye thamani ya Sh8.7 milioni kutoka maduka manne kati ya maduka saba yaliyokaguliwa katika eneo la Biashara la Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Kukamatwa kwa bidhaa hizo kunaleta shaka kwa wadau, kama kweli watu wanaohusika na bidhaa bandia watashtakiwa kwa mujibu wa sheria mpya. Kuwapo kwa sheria hiyo ni matunda ya CTI na wadau wengine ambao kwa miaka kadhaa walikuwa wanataka sheria ya bidhaa kufanyiwa marekebisho ili kudhibiti bidhaa bandia nchini.

Hata hivyo, sheria hiyo haikukidhi matarajio ya CTI na wadau wengine waliotaka kuwapo na angalizo katika bidhaa bandia. Lakini pia walitaka kuwapo na wakala maalumu ambaye atakuwa anafuatilia bidhaa bandia.

Katika muda mrefu viwanda vya kuzalisha bidhaa bandia vilijengwa kwa ajili ya mataifa fulani tu, ikiwamo Tanzania na hivyo kuangamiza bidhaa halisi za viwanda vya ndani.

Kamisheni ya Ushindani (FCC) pamoja na Shirika la Viwango nchini Tanzania (TBS) wamekuwa wakikamata bidhaa bandia kila mara.

Mwenyekiti wa CTI, Felix Mosha anasema kwamba juhudi za serikali kukabiliana na bidhaa bandia angalau zimepunguza uwapo wake katika Soko la Tanzania.

"Sisemi kuwa bidhaa bandia zimeangamizwa, lakini kwa maoni yangu bidhaa bandia zimepunguzwa kwa kiasi fulani kwenye soko la Tanzania," anabainisha.

Anabainisha kwamba hawezi kuzungumzia kiwango kwa kutumia takwimu kwa sababu CTI haijafanya utafiti.

"Hatujafanya utafiti wowote kama bidhaa hizo zimeondolewa sokoni na hili linatufanya tusipige kelele kwani hatujui ni kwa kiwango gani tatizo hilo limethibitiwa," anasema Mosha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Sekta Binafsi nchini (TPSF), Godfrey Simbeye anasema juhudi kubwa zielekezwe katika kuondoa bidhaa bandia kwani zinaathiri biashara halali na uwekezaji.

Mwaka 2009, CTI ilichapisha taarifa ambazo zimeonyesha ukiachia mambo mengine athari za bidhaa bandia kwa viwanda nchini.

Bidhaa bandia na zisizo na viwango kwa uchumi wa Tanzania, zina athari kubwa kwenye mapato, na ukusanyaji wa mapato.

Ripoti hiyo ya utafiti inaonyesha Tanzania inapoteza kati ya asilimia 15 hadi 25 ya pato la ndani kutokana na bidhaa bandia.

Hii inamaanisha kwamba serikali ilitarajia kukusanya Sh6.7 trilioni kwa mwaka 2011/2012, serikali inapata hasara ya Sh1 trilioni kutokana na bidhaa bandia zinazoingizwa nchini.

Utafiti huu umedhaminiwa na kitengo cha mazingira bora ya biashara katika ofisi ya waziri mkuu kwa kushirikiana na Best-AC na umebainisha kwamba bidhaa bandia zina mzunguko mkubwa kusababisha wafanyabiashara wa aina hiyo kutengeneza faida kubwa kuliko wale wenye bidhaa halali.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, bidhaa bandia na zile zenye viwango hafifu ambazo zinaua viwanda vya wazalendo kwa kushindwa kuwa na ushindani huru, lakini unaumiza walaji wa bidhaa mbalimbali.

**Tujadiliane kupitia ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni Bure, hautozwi!**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI